# Mirathi na Usimamizi wa Mali za Marehemu


## ISHI BAADA YA KIFO!

SIMON O. SWAI

**HAKIMU MKAZI MKUU**

**MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE – KITUO JUMUISHI CHA MAHAKAMA**

**MEI, 2025**


Posts
mira_legal_consultants
HABARI
AGOSTI 25, 2024
'NIKIFA MKE WANGU ASIOLEWE, WOSIA UHESHIMIWE'
DSM
NEWS FULL
DAILY NEWS Digital

# UKWELI WA MAISHA

- **Kifo hakikwepeki**. Miaka 100 ijayo hakuna atakayekuwa hai kati yetu (isipokuwa kwa miujiza ya Mungu!) Huu ni ukweli wa maisha!

- Kwa kuwa kifo ni dhahiri, masuala ya urithi na taratibu za mirathi huweza kujitokeza kwa lengo la kukusanya mali za marehemu, kulipa madeni yake na kugawanya mali zilizobaki kwa warithi na wanufaika.

- Kwa ujumla **maombi ya kutekeleza wosia** au **barua za usimamizi wa mirathi** ni zao la kifo.

- **Maombi ya Kutekeleza Wosia** = Hufanyika pale ambapo marehemu ameacha wosia na kutaja mtu wa kutekeleza au kusimamia wosia huo.

- **Maombi ya Barua za Usimamizi wa Mirathi** = Mazingira ambayo **mtu amefariki bila ya kuacha wosia** au **ameacha wosia bila ya kutaja jina la mtu** wa kutekeleza wosia.
  - Pale ambapo pana wosia, **maombi ya usimamizi wa mirathi huambatanishwa na wosia.**

# HATUA ZA KIMAHAKAMA

- Haki ya kurithi inafungamanishwa na haki ya kumiliki mali inayotamkwa na Ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.
  - Hivyo **huwezi kumnyima mrithi haki hii** bila uwepo wa sababu za msingi.
- Mirathi ni mchakato unaopitiwa kimahakama ili mtu anayestahili kumrithi marehemu kurithishwa kisheria mali za marehemu.
  - Haki ya kumrithi marehemu hufuata **uhusiano wa damu** (watoto kwa wazazi)**, ndoa** (mume na mke au wake) na **watoto waliosiliwa kisheria**.
  - Hata hivyo **kupitia wosia mtu ambaye haangukii kwenye makundi hayo anaweza kupata urithi kisheria**.
- Baada ya kifo na mazishi, ni **utamaduni kwa familia kufanya kikao cha familia/ukoo** na kujadili juu ya mirathi na mambo mengine yanayohusika na marehemu. **Muhtasari wa kikao huandikwa** na kuwa nyenzo mojawapo inayohitajika mahakamani.
- Cheti cha kifo ndio uthibitisho wa msingi wa tukio la kifo cha mtu. Lazima kiwasilishwe mahakamani.
  - **Cheti halisi huwasilishwa mahakamani** na **hutunzwa na Mahakama** hadi mirathi inapokamilika na **kufungwa**.

# MAHAKAMA SAHIHI YA KUFUNGUA SHAURI LA MIRATHI

- **Mahakama ya Mwanzo** husikiliza mashauri ya mirathi ambapo sheria inayotumika ni **Kiislamu** au **Kimila**.
  - Msimamizi akiteuliwa na Mahakama hii hupewa **Fomu maalumu Na. IV**
- **Mahakama ya Wilaya** imepewa mamlaka kamili ya kusikiliza mirathi ndogo **(small estate)** ikiwa na uwezo wa kuteua na kutengua msimamizi wa mirathi iwapo sheria inayotumika siyo ya Kiislamu wala Kimila.
- **Hakimu Mwenye Hadhi Maalumu (**Court of District Delegate) Amepewa mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mirathi ambayo siyo mirathi ndogo. Mirathi yenye makadirio ya thamani ya Tsh 100,000,000/= na zaidi husikilizwa na hakimu mwenye hadhi maalumu.
- **Mahakama Kuu** haina ukomo wa kusikiliza mashauri ya mirathi.
  - Msimamizi akiteuliwa na Mahakama hii hupewa Fomu maalumu **Form No. 66** (kama kuna wosia)au **68** (kama hakuna wosia).



# WOSIA

- Mtu anapofariki bila ya kuacha wosia mirathi yake husimamiwa kwa kuzingatia sheria husika.
  - Marehemu **Muislamu** sheria za Kiislamu zitatumika.
  - Marehemu aliyeishi **Kimila** mitahi itazingatia mila na tamaduni za jamii husika, na
  - Kwa marehemu ambaye hakuwa akifuata sheria tajwa hapo juu, mirathi yake itazingatia **sheria za nchi** kama Indian Succession Act, Hindu Wills Act Nk.
- **Wosia** ni **tamko la hiari la mtu anayeishi** juu ya mali zake na nia yake **juu ya usimamizi** wa mali hizo au **mgawanyo wake** kwa warithi na wanufaika **baada ya kifo chake**.
  - Wosia hufanya **kazi baada ya kifo cha mwenye kutoa wosia**. Haifai kuogopa kuandika wosia wala kutafsiri kama ni laana au uchuro.
- Kuna aina **kuu mbili** za wosia;
  - (i) Wosia wa Mdomo na
  - (ii) Wosia wa Maandishi.
- Mtekeleza wosia au msimamizi wa mirathi **hana nafasi ya kutekeleza kinyume na wosia**.

# SIFA ZA WOSIA HALALI

- Wosia ni tamko la kisheria na hivyo **lazima likidhi vigezo** vya kisheria ili **uwe halali**;
  - (i) Jina kamili na sahihi la mtoa wosia,
  - (ii) majina ya **warithi** na au **wanufaika**,
  - (iii) Jina au majina ya watekeleza wosia (siyo lazima sana ila ni vizuri),
  - (iv) Orodha na maelezo *(description)* ya mali unazomiliki,
  - (v) Mgawanyo wa mali kwa warithi na au wanufaika,
  - (v) Tarehe
  - (vi) Saini ya mwenyekutoa wosia na
  - (vii) Majina na saini za **mashahidi angalau wawili**, mmojawapo lazima awe **ndugu wa mwenyekutoa wosia.**
- Sheria hailazimishi mahali pa kuhifadhi wosia.Hata hivyo, **RITA** ni wakala maalumu wa Serikali anayetoa huduma za **uandishi** na **utunzaji wa wosia**.

# KUKUSANYA NA KUGAWANYA MALI ZA MAREHEMU

- Sheria inamtaka msimamizi wa mirathi **kukusanya** mali za marehemu, **kulipa madeni** yake na **kugawa mali kwa warithi**.
  - **Orodha kamili** ya mali za marehemu na mgawanyo vinapashwa kusajiliwa mahakamani **ndani ya miezi minne** kwa Mahakama ya mwanzo na **ndani ya miezi sita** kwa Mahakama Kuu na Wilaya.
- **Hesabu ya mgawanyo** wa mali za marehemu inapashwa kusajiliwa mahakamani ndani ya **miezi kumi na mbili** kwa kwa Mahakama Kuu na Wilaya.
- Fomu Mahsusi za kukusanya mali na kugawa ni;
  - **Fomu Na. V (orodha)** na **Na. VI (hesabu)** – Mahakama ya mwanzo.
  - **Fomu Na. 80 (orodha)** na **No. 81 (hesabu)** – Mahakama Kuu na Wilaya.
- **Hisa** (shares) na pesa kwenye mitandao **ni sehemu ya mali za marehemu** ambazo **zapashwa kuwepo kwenye orodha ya mali** za marehemu.
  - **Usajili wa hisa kwa majina sahihi** ni **jambo la msingi** sana kwa kuwa lina athari kubwa kwenye hatua za **kurithisha.**
  - **Usajili wa hisa kwa majina ya watu wengine** kunapelekea mali hiyo kukosa sifa za kuwa kwenye orodha ya mali za marehemu na Mahakama haiwezi kutoa amri ya kurithisha.
- Msimamizi anawajibika kumilikisha mali zote za marehemu kwa warithi au wanufaika.

# USIRI & USAJILI WA MALI KWA MAJINA TOFAUTI AU YASIYO SAHIHI

- Barua za kutekeleza wosia au kusimamia mirathi hutolewa **kwa majina ambayo marehemu amesajiliwa kwenye cheti cha kifo.**
  - Ni muhimu sana kupata cheti cha marehemu kwa majina yake halisi na kamili.
- Daudi John Mussa – **David Yohana** Mussa
- Christina John Mussa – **Tina** John Mussa
- Kumiliki hisa au mali kwa siri hakuna manufaa kwako wala warithi wako wakati umefariki. **Hii ni sawa na mali iliyopotea,** Jasho lako la kutafuta mali hiyo litapotea bure.
- Tumia **wosia kulinda mali zako za siri**, kisha endelea kumiliki mali hizo salama kwa siri.

# MALI ZA NDOA KWENYE MIRATHI


- Ndoa **hukoma kinapotokea kifo cha mwanandoa** mmoja.
  - Kwa msingi huo **hakuna nafasi ya kujadili** tena masuala ya ndoa baada ya kifo**.**
  - Kwa mazingira hayo sheria za mirathi hushika hatamu.
- Kwenye kifo cha mwanandoa mmoja, **mali huhesabika ni za mwanandoa yule ambaye imesajiliwa kwa jina lake**.
  - Mwanandoa anayebaki hai **anakuwa na haki ya kumrithi mwenzi wake** aliyefariki kwa kuzingatia sheria husika, yaani; Kiislamu, Kimila au sheria za Serikali.
    - Mfano; endapo unadai kuwa na mchango kwenye chumo la ndoa na kuweka madai yako kwenye shauri la mirathi, tatizo lililopo ni kwa namna gani utathibitisha mchango huo bila uwepo wa mwenzi wako na kama ni halali kisheria kuthibitisha mbele ya msimamizi wa mirathi.
- Fikiria juu ya **Umiliki Pacha** (Joint Tenancy), kinapotokea kifo cha mmoja, umiliki huamia kwa mwanandoa anayeishi dhidi ya yeyote. Mali hii **haiwezi kuingizwa kwenye mirathi** na
- **Umiliki wa Pamoja** (Tenancy in Common) ambapo kwenye kifo cha mwanandoa mmoja ni sehemu ya umiliki wake pekee huingia kwenye mirathi.

# MFANO WA MALI INAYOPOTEA KWA WARITHI KUTOJULIKANA

- Kwa miaka 13 jumla ya **TZS 970,011,736.51** haikufikia warithi. Hii inatoa wastani wa fedha zinazopotea kwa mwaka kuwa **TZS 74,616,287.42**

- Pangilia mali zako leo na usiache nguvu zako zipotee bure pale unapofariki.

- **Andika wosia leo, Kesho hatuna uhakika nayo!**



# MWISHO

*"Ardhi ni mali ya wanaoishi kwa haki ya matumizi; wafu hawana mamlaka wala haki juu yake." "Ingekuwa kizazi kimoja kingeweza kufunga kingine, wafu na sio walio hai wangetawala."*

*Barua kutoka kwa James Madison kwenda kwa Thomas Jefferson (Rais wa nne na Rais wa tatu wa USA mtawalia), 1789*

asante sanaa.